LITURGHIA TAKATIFU

iliyoandikwa na
Yohana Krisostomo

Orthodox Editions

ORTHODOX CHURCH

PATRIARCHATE OF ALEXANDRIA

HOLY ARCHBISHOPRIC OF IRINOUPOLIS (East Africa)

"Orthodox Editions", P.O.Box 46119, Nairobi,KENYA

Translated by:

The Translation Committee of the Holy Archbishopric of Irinoupolis.

Provisional Edition - 1985

Edited by:

- Inter-Orthodox Missionary Centre "Porefthendes", Athens.
- Apostoliki Diakonia of the Church of Greece - Foreign Mission Office, Athens.

L I T U R G H I A   T A K A T I F U

iliyoandikwa na

Yohana Krisostomo

ORTHODOX EDITIONS

Yohana Krisostomo Mtakatifu

UTANGULIZI

Mazoezi ya mitume, ambayo yalisaidia Ekklesia (Kanisa) ya kikristo kukuza, haikuegamia ujuzi wa mafundisho ya akili au sheria mpya, lakini iliegamia hasa nafsi ya Yesu Kristo na uwezo wa kufufuka kwake. Bwana alichagua wajumbe wa kwanza wa Ekklesia yake, ni mitume "ila wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, tena wawe na amri ya kutoa pepo".

Na kitu cha kwanza kilikuwa walio wake wafanye ni "wapate kuwa pamoja naye", kuwa kwendelea katika uhusiano wa kuishi katika yeye. Kristo, kabla ya kusulubishwa msalabani, kwa ajili ya kuhakikishia ushirika pia katika wakati ujao, aliwatolea mitume Fumbo ya Shukrani ya umungu (Mt 26:26-29; Mk 14:22-25; Lk 22:14-20).

Mitume walifuata amri hii ya Bwana, "fa-

nyeni hivi kwa ukumbusho wangu". Waliitunza katika maisha yao yote na katika vitendo vyao vyote na waliipokezana kizazi kwa kizazi (1 Kor 11:23-24). Wakati wa kukuzwa wa Ekklesia la mwanzo, maneno mengine yalitoka katika Agano la Kale na Jipya, na pia maombi na ishara viliongeza kwa kiini cha mwanzo. Katika mwanzo wa karine ya nne kutoka na hayo maandiko ya Liturghia takatifu iliandikwa na baba Yohana Krisostomo na ikapewa jina lake.Kutoka hapo na wakati wote zaidi ya karine kumi na sita maandiko haya hayakubadilishwa.

Mazoezi ya mitume ya ujuzi wa nafsi ya Kristo na ya "ushirika" na Yeye yaendelea kuwa mazoezi ya maisha katika Ekklesia. Na mazoezi haya yaonyesha na kulinda na maisha katika kuabudu kwa Ekklesia.

Hasa Liturghia takatifu ni:

- kumbuka kwa kuzaliwa, kwa maisha, kwa kufa msalabani na kufufuka kwake Kristo, kwa kupaa mbinguni kwake, kwa kukaa kwake kwa kuume kwa Baba, na kwa kuja kwake mara ya pili katika utukufu;
- sakada ya fumbo ("Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu... hii ndiyo damu yangu ya aga-

no jipya, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi"- Mt 26:26-28);

- ushirika na Bwana aliyehai ("Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele" - Jn 6:56);

- shukrani kwa ajili ya upendo wa Mungu usio na mpaka. Gauana katika shukrani iliyotolewa na Ndugu yetu aliye mzaliwa wa kwanza ("... akashukuru, akaumega, akawapa,..." - Lk 22:19);

- ukiri wa imani yetu katika nguvu ya kifo chake Bwana cha ukombozi (1 Kor 11:26).

* *

Kila Liturghia takatifu ifanyikapo kufahamu kwa "ufalme wa Mungu" kuwa kupya - mahali tulipo na ndani yetu:

Kwanza, Liturghia takatifu ufunua kifupi maana ya historia, ambayo ni ugeuzo wa kiumbe, ugeuzo wa ulimwengu katika upendo wa Neno wa Mungu na katika kitendo cha Roho Mtakatifu.

Pili, Liturghia takatifu ni mwito wa mwendo wa kukombolewa toka tamaa ya kila namna mbaya, kuogopa, udhaifu, kupenda makosa na u-

tumwa wa ubinafsi wetu.

Tatu, Liturghia takatifu lyaongoza katika ushirika wa upendo na waumini wa wakati wote na wa mahali po pote, kwa kuleta nguvu ya kufahamu kwa umoja uliokuwa na watu wote.

Pia, nne, mkutano wa waumini wa sadaka ya shukrani, kama "alama" ya Ufalme wa mbinguni, ni ungamo mkuu kwa ulimwengu, na furaha nyingi tena shangwe, ni mwito kwa ushirika wa upendo pamoja naye aliye Upendo, aliye Mungu wa Utatu.

Hivyo, tukio la sadaka ya shukrani katika Liturghia Takatifu lathibitisha ya ukristo na ni kipeo cha juu ya mazoeo; lageuza maisha na kuyafanya mgawanyo wa utukufu wa Mungu. Uchaji, na zaidi Liturghia takatifu uasaidia na kuendeleza kuingiza kwa "Evangelio ya neema" na ya uokovu; si kama mafundisho ya akili, ila kama nguvu. Liturghia takatifu ni habari katika utukufu na ni uonyesho wa Ufalme wa mbinguni kwa ulimwengu, ambao, ijapokuwa uataka kutoujali, kwa kiini kuutafuta.

* *

Muhuri wa Liturghia takatifu umewekwa

kwa kiroho kiorthodhoksi na kwa kufahamu kwa kiorthodhoksi. Liturghia takatifu ilikuwa na ipo tegemeo, chemchemi ya uzima na baraka kwa kila mworthodhoksi, kwa mtu mwenye busara na asiye na ujuzi, kwa mtu mwenye nguvu na asiye nazo, kwa mtu wa mjini na mtu mashambani. Kwa karine nyingi yaunganisha waumini katika ushirika wa siri, mtakatifu, jawa na akili za maisha ya milele na ya uhuru wa roho.

Liturghia takatifu yaletwa kanisani na kusudi ya kuendelea katika maisha ya nafsi ya kila mkristo, na ya kutakaswa kila mawazo, kila nia na kila kitendo, jinsi ya jitihada kutolea nafsi yake "dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu" (Rom 12:1).

Liturghia takatifu si tamasha wala kusikia, lakini ni kitendo cha umungu, kitendo cha Mungu na mungano katika watu na Mungu,(Katika kiyunani maana ya neno "liturghia" ni kitendo na watu na kwa ajili ya watu). Kwa hiyo Ekklesia yetu yatuita kushiriki kati Liturghia takatifu, si kama kutazama, ila kufanya tendo takatifu pamoja na kasisi.

Katika Liturghia takatifu mwumini apata kuwa mpya, atangua ushawishi mbaya na vimhata-

rishavyo; jinsi hivyo mwumini apata nguvu mpya ya kuendelea katika njia yake, akiwa "wa mwili mmoja na wa damu moja" na Kristo, ili arudie maisha ya kila siku,

. akiwa mnyenyekevu zaidi na mpole zaidi katika uhusiano na watu wengine,

. mjasiri wa shujaa zaidi na bila kutegemea faida katika upendo,

. mwangavu zaidi na kwa mwanga wa ufufuko katika tazamo lake na kuishi kwake,

. mthabiti kudai katika maisha ulio mwangaza mkuu wa mtu: kuendelea kwa hamu ya mwisho alivyoumbwa, maana afike kuwa "kwa sura" ya Kristo, mwenye Roho Mtakatifu katika maisha ya jamii, wakili wa maendeleo ya nchi yake na kawaida ya utu kwa hamu ya mwisho wake, kwa ushirika wa upendo na kielezo cha Utatu Mtakatifu.

Askofu Prof. ANASTASIOS YANNOULATOS

L I T U R G H I A   T A K A T I F U

A

LITURGHIA YA WAKATIHUMENO

SHEMASI Ee Padri, himidi. — Εὐλόγησον, Δέσποτα.

KASISI Mhimidiwa ni ufalme wa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Εὐλογημένη ἡ βασιλεία...

WATU Amina.

SALA KUBWA YA AMANI (IRINIKA)

SHEMASI Kwa amani tumwombe Bwana. — Ἐν εἰρήνῃ τοῦ Κυρίου...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya amani kutoka juu na ya wokovu wa roho zetu, tumwombe Bwana. — Ὑπὲρ τῆς ἄνωθεν εἰρήνης...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya amani ya dunia yote, na kusimama imara kwa Ekklesia (Kanisa) takatifu ya Mungu, na ya umoja wa wote, tumwombe Bwana. — Ὑπὲρ τῆς εἰρήνης τοῦ...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya nyumba hii takatifu na waingiamo kwa imani, heshima na kumcha Mungu, tumwombe Bwana. — Ὑπὲρ τοῦ ἁγίου οἴκου...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya Askofu wetu mkuu *(jina)* mheshimiwa, na makasisi wetu, mashemasi, ya wateule na ya watu wote, tumwombe Bwana. — Ὑπὲρ τοῦ Ἀρχιεπι-σκόπου...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya taifa letu, na raisi wetu, na viongozi wetu, na wa maje-shi wapendao dini, tumwombe Bwana. — Ὑπὲρ τοῦ εὐσεβοῦς ἡμῶν...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya mji huu na miji yote na nchi zote na waishimo kwa ima-ni, tumwombe Bwana. — Ὑπὲρ τῆς πόλεως ταύτης...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya majira mema ya mwaka kupata mvua ya kutosha na hewa safi na rutuba yakutosha kwa ardhi, tumwombe Bwana.

Ὑπέρ εὐκρασίας ἀέρων...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya wasafiri hewani, juu baharini majini na nchini kavu, na kwa ajili ya wagonjwa na wachoshwa na mateka kupata uhuru, na kwa ajili ya wokovu wao, tumwombe Bwana.

Ὑπέρ πλεόντων, ὁδοιπορούντων...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya kuokolewa kwa kila sikitiko, ghadhabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana.

Ὑπέρ τοῦ ῥυσθῆναι ἡμᾶς...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, Ee Mungu, kwa neema yako.

Ἀντιλαβοῦ, σῶσον, ἐλέησον...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa zaidi kushinda wote, Bibi wetu mtukufu,

Τῆς παναγίας, ἀχράντου,...

Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, hata sisi pia wenyewe na kila mmoja wetu na wenzetu wote, hata maisha yetu, kujiweka mikononi mwa Kristo Mungu.

WATU Kwako, Ee Bwana.

Sala ya Itikio (Antifono) ya 1

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, Mungu wetu, mwenye enzi yote na utukufu kupita kila ufahamu; uliye na huruma sana, tena na upendo kwa wanadamu usioelezeka; wewe ndiwe, Bwana wa Mabwana, kulingana na huruma yako utazame sisi na hekalu hii takatifu na utupatie sisi pamoja nao tunaokuomba huruma yako ya utajiri na rehema zako.

Κύριε ὁ Θεὸς ἡμῶν, οὗ τὸ...

kwa sauti

Kwa kuwa utukufu wote, na heshima, na usujudu ni haki yako, ya Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

Ὅτι πρέπει σοι πᾶσα δόξα...

WATU Amina.

Tunaimba Itikio. Kila Jumabwana au katika sikukuu za watakatifu tunaimba viitikio hivi:[1]

MSOMAJI (Zab.103:1) Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Naam, vyote vilivyo ndani yangu vilihimidi jina lake takatifu.

WATU Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, Ee Mwokozi, utuokoe.

Ταῖς πρεσβείαις τῆς Θεοτόκου...

MSOMAJI (Zab.103:2) Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili zake zote.

WATU Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, Ee Mwokozi, utuokoe.

MSOMAJI (Zab.103:19) Bwana ameweka kiti chake cha enzi mbinguni, na ufalme wake unavitawala vitu vyote.

---

1. Toka Jumabwana ya Paskha mpaka siku kabla ya Kupaa kwake Kristo mbinguni, katika kila siku na kila Jumabwana, tunaimba viitikio hivi:

(Zab.66:1) Mpigie Mungu kelele za shangwe, nchi yote. Kwa maombi...

(Zab.66:2) Imbeni utukufu wa jina lake, tukuzeni sifa zake. Kwa maombi...

(Zab.66:3) Mwambieni Mungu, matendo yako

WATU Kwa maombi ya Mzazi-Mungu, Ee Mwokozi, utuokoe. — Ἔτι καὶ ἔτι ἐν εἰρήνῃ...

SHEMASI Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, Ee Mungu, kwa neema yako. — Ἀντιλαβοῦ, σῶσον, ἐλέησον...

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa zaidi kushinda wote, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, hata sisi pia wenyewe na kila mmoja wetu na wenzetu wote, hata maisha yetu, kujiweka mikononi mwa Kristo Mungu. — Τῆς παναγίας, ἀχράντου,...

WATU Kwako, Ee Bwana.

Sala ya Itikio (Antifono) ya 2

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, Mungu wetu, uwaokoe watu — Κύριε ὁ Θεὸς ἡμῶν, σῶσον...

---

yatisha kama nini! Kwa maombi...

wako na kubariki urithi wako; ulinde jamii ya Ekklisia lako; tena utakase hao wanaopenda uzuri wa nyumba yako; wewe uwape utukufu kwa uweza wako wa umungu, na usijitenge nasi tunaotumaini wewe.

kwa sauti

Kwa kuwa utawala ni kwako, na ufalme, na uweza, na utukufu ni vyako, wa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

῞Οτι σόν τό κράτος...

Tunaimba Itikio. Kila Jumabwana au katika sikukuu za watakatifu tunaimba viitikio hivi:[1]

MSOMAJI (Zab.146:1-2) Ee nafsi yangu, u-

---

1. Toka Jumabwana ya Paskha mpaka siku kabla ya Kupaa kwake Kristo mbinguni, katika kila siku na kila Jumabwana, tunaimba viitikio hivi:

(Zab.67:1a) Mungu na atufadhili na kutubariki. Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, ...

(Zab.67:1b) Kutuangazie uso wake na kutuhurumia. Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, ...

msifu Bwana. Nitamsifu Bwana muda ninaoishi, nitamwimbia Mungu wangu ningali ni hai.

WATU Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, sisi twakuimbiao, Alleluia[1]. Σῶσον ἡμᾶς, Υἱὲ Θεοῦ,...

MSOMAJI (Zab.146:5) Heri ambaye Mungu wa Yakobo ni msaada wake, na tumaini lake ni kwa Bwana, Mungu wake.

WATU Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, sisi twakuimbiao, Alleluia.

MSOMAJI (Zab.146:10) Bwana atamiliki milele, Mungu wako, Ee Sayuni, kizazi hata kizazi.

WATU Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, sisi twakuimbiao, Alleluia.

(Zab.67:2) Njia yake ijulike duniani, wokovu wake katikati ya mataifa yote. Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, ...

1. *Siku za wiki isio Jumabwana twaimba:*

Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, uliyeajabu katika watakatifu,sisi twakuimbiao, Alleluia.

Utukufu kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. — Δόξα Πατρί καί Υἱῷ...

Sasa na sikuzote, hata milele na milele. Amina.

Ee Mwana wa pekee tena Neno wa Mungu, ukiwa usiyekufa ukakubali kwa ajili ya wokovu wetu kupata mwili kwa Maria Mzazi-Mungu (Theotokos) tena Bikira daima, ukawa mtu bila kujigeuza; na ukasulubiwa, Ee Kristo Mungu, ukakanyaga kifo kwa kifo; uliye mmoja wa Utatu Mtakatifu, na watukuzwa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, utuokoe. — Ὁ μονογενής Υἱός...

SHEMASI Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana. — Ἔτι καί ἔτι ἐν εἰρήνῃ...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, Ee Mungu,kwa neema yako. — Ἀντιλαβοῦ, σῶσον,...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa zaidi kushinda wote, Bibi wetu mtukufu, — Τῆς παναγίας, ἀχράντου,...

Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, hata sisi pia wenyewe na kila mmoja wetu na wenzetu wote, hata maisha yetu,kujiweka mikononi mwa Kristo Mungu.

WATU Kwako, Ee Bwana.

Sala ya Itikio (Antifono) ya 3

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, uliyetupatia sala hizi za pamoja; uliyeahidi kwa watu wawili hata kwa watu watatu hao wanaopatana katika jina lako, kusikiliza na kuzitimiza dua zao; wewe ndiwe utimize dua za watumwa wako kwa faida yetu, ukitupatia ujuzi wa kujua kamili ukweli wako katika dunia hii, tena uzima wa milele katika ulimwengu utakaokuja. Ὁ τάς κοινάς ταύτας...

kwa sauti

Kwa kuwa wewe u Mungu mwema na mpenda-wanadamu, na kwako tunatoa utukufu, kwa Baba, na Mwana, na Ro- Ὅτι ἀγαθὸς καὶ...

ho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

WATU Amina.

KUINGIA KUDOGO (MIKRA ISODHOS)

Kila Jumabwana tunasoma Itikio na tunaimba Apolyitikio ya Sauti ya Jumabwana.

Itikio:

(Zab.118:24) Siku hii ndiyo aliyoifanya Bwana, tutashangilia na kuifurahia.

Wakati wa kuimba Apolyitikio[1]*, kuingia kudogo kunafanywa.*

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Tumwombe Bwana. Bwana, hurumia. Τοῦ Κυρίου δεηθῶμεν.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana wa Mabwana, Mungu wetu, uliyeweka mbinguni makundi na majeshi ya Malaika, na Malaika majemadari kuadhimisha utukufu wako; ufanye kuingia kwetu kuwe pamoja na Δέσποτα Κύριε, ὁ Θεός...

---

1. Siku za wiki isio Jumabwana twaimba Apolytikio ya mtakatifu wa siku.

Malaika watakatifu, wanaoadhimi-sha pamoja nasi, na pamoja nasi kutoa utukufu kwa wema wako. Kwa kuwa kila utukufu, na heshima, na usujudu ni haki yako, ya Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Ee Padri, bariki Kuingia takatifu. Εὐλόγησον, Δέσποτα,...

KASISI *kwa sauti ya upole anabariki kwa mkono wake*

Kubarikiwa kuwe Kuingia kwa pata-katifu pako, daima, sasa na siku-zote, hata milele na milele. Εὐλογημένη ἡ εἴσοδος...

SHEMASI Amina.

SHEMASI *kwa sauti*

Hekima! Simameni wima! Σοφία. Ὀρθοί.

WATU Njoni tumsujudie na kumwangukia Kristo; utuokoe, Ee Mwana wa Mu-ngu, uliyefufuka katika wafu, sisi twakuimbiao, Alleluia[1]. Δεῦτε προσκυνή-σωμεν...

---

1. Siku za wiki isio Jumabwana twaimba:

Njoni ...; utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, uli-

Tunaimba Apolyitikio, na Apolyitikio ya Hekalu. Tena Kontakio:[1]

Wewe uliye himaya ya Wakristo isiyoaibika; uliye mpatanishi daima kwa Mwumba; usidharau sauti za maombi yetu sisi wenye dhambi; lakini, wewe uliye mwema, uje na kutusaidia, sisi tunaopaza sauti kwako. Haraka kututetea na kutuombea kwa Mungu sisi tunakuomba, wewe uliyehami daima hao wanaokuheshimu, Ee Mzazi-Mungu (Theotokos).

WIMBO WA TAKATIFU TATU (WIMBO TRISAGHIO)

Baada ya Kuingia kudogo na matropari

SHEMASI Tumwombe Bwana. Τοῦ Κυρίου δεηθῶμεν.

---

ye mtenda-miujiza katika watakatifu, sisi twakuimbiao , Alleluia.

Toka Paskha mpaka Kupaa kwake Kristo mbinguni, twaimba:

Mhimidini Mungu katika mikutano (Makanisa), Bwana katika chimbuko ya Israeli. Utuokoe, Ee Mwana wa Mungu, uliyefufuka katika wafu, sisi twakuimbiao, Alleluia.

1. *Ikiwa sikukuu haina Kontakio.*

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

KASISI *kwa sauti*

Kwa kuwa wewe ndiwe mtakatifu, Ee Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu, kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, — Ὅτι ἅγιος εἶ ὁ Θεός...

SHEMASI Hata milele na milele. — Καὶ εἰς τοὺς...

WATU Amina.

Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Usiyekufa Mtakatifu, utuhurumie. *(x 3)*[1] — Ἅγιος ὁ Θεός,...

Utukufu kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. — Δόξα... Καὶ νῦν...

Sasa na sikuzote, hata milele na milele. Amina.

Usiyekufa Mtakatifu, utuhurumie.

SHEMASI Kwa nguvu. — Δύναμις.

---

1. *Jumabwana ya Paskha na katika sikukuu za Bwana Jesu Kristo tunaimba:*

(Gal.3:27)

Ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Alleluia.

WATU Mungu Mtakatifu, Mweza Mtakatifu, Usiyekufa Mtakatifu, utuhurumie.

Tukiimba wimbo wa takatifu tatu (Wimbo Trisaghio), kasisi anasali kwa mnong'ono hivi

KASISI Ee Mungu, uliye Mtakatifu, na kukaa ndani ya watakatifu; unayesifiwa kwa sauti takatifu tatu na Waserafi, tena waadhimishwa na Waheruvi, na kusujudiwa na Nguvu zote za mbinguni juu; uliyefanya vitu vyote kwa ubure, na vikawa; uliyemwumba binadamu kwa sura na mfano wako, tena kumpamba kwa vipaji vyako vyote; unayempa ye yote anayekuuliza hekima na busara, usiyemdharau mwenye dhambi kumuacha apotee, bali uliweka kutubu, ili apate wokovu; uliyestahilisha hata sisi watumwa wako wanyenyekevu na wasiostahili, hata wakati huu kusimama mbele ya utukufu wa madhabahu yako matakatifu na kukuletea kusujudu na sifa iliyo haki zako; wewe Bwana wa Mabwana, upo-

Ὁ Θεὸς ὁ Ἅγιος, ὁ ἐν ἁγίοις...

kee wimbo huu wa takatifu tatu (wimbo trisaghio) tunautoa kwa midomo yetu, sisi wanadamu wenye dhambi, na utupatie neema yako. Utusamehe kila dhambi tumeifanya kwa hiari ama si kwa hiari; utakase roho na miili yetu; na utustahilishe kukuabudu kwa utakatifu siku zote za maisha yetu; kwa maombi ya Mzazi-Mungu wetu mtakatifu, na watakatifu wote waliokupendeza tangu milele.

Kwa kuwa wewe ndiwe Mtakatifu, Ee Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu, kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Ee Padri, amri. Κέλευσον, Δέσποτα.

KASISI *kwa mnong'ono*

Abarikiwe yeye ajaye kwa jina la Bwana. Εὐλογημένος ὁ...

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Ee Padri, himidi kiti cha enzi kilicho juu. Εὐλόγησον, Δέσποτα,...

KASISI *kwa mnong'ono*
Mhimidiwa ni wewe,uliye katika kiti cha enzi cha ufalme wako,uketiye begani pa Waheruvi, daima, sasa na sikuzote,hata milele na milele. — Εὐλογημένος εἶ, ὁ...

SHEMASI Amina.

MASOMO

SHEMASI Tusikilize. — Πρόσχωμεν.

MSOMAJI *anasoma mstari ya Prokeimeno*

SHEMASI Hekima. — Σοφία.

MSOMAJI Somo katika waraka (wa kwanza *au* wa pili) wa Paulo (*au* Yakobo,n.k.) (*au* katika Matendo ya Mitume), sura..., mstari... .

SHEMASI Tusikilize. — Πρόσχωμεν.

Msomaji anasoma kwa sauti kimuziki.

Shemasi analeta chetezo kwa kasisi.

SHEMASI *kwa mnong'ono*
Ee Padri, bariki uvumba.

KASISI *kwa mnong'ono*
Mhimidiwa ni Mungu wetu daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. Amina.

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Tumwombe Bwana. Bwana, hurumia.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana wa Mabwana, mpenda-wana-damu, wangaze mioyoni mwetu na nuru yako takatifu ya ujuzi wa kujua Mungu; tena ufungue macho ya fikira zetu, ili tufahamu mahubiri ya Evangelio yako. Uweke ndani yetu uchaji wa amri zako, kusudi tupate kuzikanyaga tamaa mbaya zote za kimwili, na kufuata njia ya kuishi kiroho, hata kufikiri na kutenda vitu vyote vinavyokupendeza. Kwa kuwa wewe ndiwe mwangazo wa roho na miili yetu, Ee Kristo Mungu, na kwako tunatoa utukufu, pamoja na Baba wako asiye na mwanzo, na Roho Mtakatifu kamili, mwema na mpaji wa uhai, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

Amina.

Ἔλλαμψον ἐν ταῖς καρδίαις ἡμῶν,...

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Ee Padri, bariki msomaji wa Evangelio takatifu wa (Mathayo, Mariko, Luka,Yohana), Mtume mtakatifu,msifiwa na mwandikaji wa Evangelio.

KASISI *anambariki na kumpa Evangelio*

Kwa maombi ya (Mathayo, Mariko, Luka, Yohana), Mtume mtakatifu, msifiwa na mwandikaji wa Evangelio, Mungu akupe neno, wewe uliye msomaji wa evangelio, na akumpe nguvu kubwa, kutimiliza evangelio ya Mwanae mpendwa, tena Bwana wetu, Yesu Kristo.

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Amina. Amina. Amina. Na iwe kwangu sawasawa kwa neno lako. Εἰρήνη σοί τῷ...

Msomaji amalizapo kusoma waraka

KASISI Amani kwako, ee msomaji (hata kwa watu wote).

WATU Alleluia. Alleluia. Alleluia. Ἀλληλούϊα,...

KASISI Hekima. Simameni wima. Tusikilize Σοφία. Ὀρθοί...

	Evangelio takatifu. Amani kwa wo-te.	Εἰρήνη πᾶσι.
WATU	Na iwe kwa roho yako.	Καὶ τῷ πνεύματί σου.
SHEMASI	Somo katika Evangelio takatifu i-liyoandikwa na (Mathayo, Mariko, Luka, Yohana), sura ..., mistari	Ἐκ τοῦ κατά...
KASISI	Tusikilize.	Πρόσχωμεν.
WATU	Utukufu kwako, Ee Bwana, utukufu kwako.	Δόξα σοι, Κύριε,...

Shemasi anasoma vizuri sehemu ya Evangelio kimuziki.

Shemasi amalizapo kusoma Evange-lio:

KASISI	Amani kwako, ee msomaji wa Evange-lio.	Εἰρήνη σοί τῷ...
WATU	Utukufu kwako, Ee Bwana, utukufu kwako.	Δόξα σοι, Κύριε,...

LITANIA NDEFU (EKTENÍ)

SHEMASI	Tuseme sisi sote kwa roho yetu yo-te na kwa mawazo yetu yote, tuseme.	Εἴπωμεν πάντες...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)*

SHEMASI Ee Bwana mwenyezi, Mungu wa mababa wetu, tunakuomba, utusikilize na kutuhurumia.

Κύριε, Παντοκράτορ,...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)*

SHEMASI Utuhurumie, Ee Mungu, kadiri ya huruma yako kubwa, tunakuomba, utusikie na kutuhurumia.

Ἐλέησον ἡμᾶς, ὁ...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)*

SHEMASI Tena tunakuomba kwa ajili ya wakristo watauwa waorthodhoksi wote.

Ἔτι δεόμεθα ὑπὲρ τῶν εὐσεβῶν...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)*

SHEMASI Tena tunaomba kwa ajili ya Askofu wetu mkuu *(jina)*

...ὑπὲρ τοῦ Ἀρχιεπισκόπου...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)*

SHEMASI Tena tunaomba kwa ajili ya ndugu zetu makasisi, mashemasi, watawa na udugu wetu katika Kristo.

...ὑπὲρ τῶν ἀδελφῶν...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)*

SHEMASI Tena tunaomba kwa ajili ya watumwa wa Mungu, watauwa wakristo wote

...ὑπὲρ ἐλέους,...

orthodhoksi, wanaokaa au kupita katika mji huu na nchi hii, washarika, wasimamizi, wanaoweka wakfu katika nyumba hii takatifu, ili wapewe huruma, uzima, amani, afya, wokovu, msaada , msamaha na maondoleo ya dhambi.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).(3)

SHEMASI Tena tunaomba kwa ajili ya warehemiwa wajengaji wa nyumba hii takatifu, ambao ni kwa makumbusho heri, hata ya baba na ndugu zetu zote orthodhoksi warehemiwa, ambao wamelala hapa na mahali po pote. ...ὑπέρ τῶν μακαρίων...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).(3)

SHEMASI Tena tunaomba kwa ajili yao wanaotenda matendo mema katika nyumba hii takatifu na heshimiwa, kwa ajili yao wenye juhudi, wanaoimba hata ya watu wote waliosimama hapa, wakingoja huruma yako kubwa na ya utajiri. ...ὑπέρ τῶν καρποφορούντων...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).(3)

Sala ya litania ndefu (ektenî)

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, Mungu wetu, upokee maombi marefu haya ya watumwa wako, na utuhurumie kadiri ya wingi wa huruma yako; na utupatie rehema zako, sisi na watu wako hawa wanaongoja huruma yako ya utajiri.

Κύριε, ὁ Θεός ἡμῶν, τὴν ἐκτενῆ...

kwa sauti

Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu mrahimu na mpenda-wanadamu; na kwako tunatoa utukufu, kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

Ὅτι ἐλεήμων...

WATU Amina.

Ἀμήν.

MAOMBI KWA AJILI YA WAKATIHUMENO (WANAFUNZI WA UBATIZO)

SHEMASI Enyi wakatihumeno, ombeni kwa Bwana.

Εὔξασθε, οἱ κατηχούμενοι, τῷ Κυρίῳ...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Hata sisi tulioamini kwa ajili ya wakatihumeno tumwombe Bwana.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Ili Bwana awahurumie.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Awafahamishe neno la ukweli.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Awafunulie Evangelio la haki.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Awaunganishe na Ekklisia lake takatifu, moja na la ki-mitume.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Uwaokoe, uwahurumie, uwasaidie, uwahifadhi, Ee Mungu, kwa neema yako.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Enyi wakatihumeno, inameni vichwa vyenu kwa Bwana.

Οἱ κατηχούμενοι, τάς κεφαλάς ὑμῶν...

WATU Kwako, Ee Bwana.

Mbele ya kufungua Antiminsio

Sala ya kuwaombea kwa Mungu

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, Mungu wetu, unayekaa juu, na kuona viumbe vya unyenyekevu; uliyetumia watu wokovu huo, ndiye Yesu Kristo Mungu Bwana

Κύριε, ὁ Θεός ἡμῶν, ὁ ἐν ὑψηλοῖς...

wetu, Mwana wako pekee, waangalie watumwa wako, wakatihumeno, walioinama shingo zao mbele yako; wastahilishe kuzaliwa mara ya pili, na kupewa maondoleo ya dhambi na uvazi usiovunda; waunganishe na Ekklisia lako takatifu,moja na la mitume; na uwahesabie katika kundi lako lililochaguliwa.

kwa sauti

Ili hata hawa pamoja nasi walitukuze jina lako adhimu na linaloheshimiwa, la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote,hata milele na milele. — Ἵνα καί αὐτοί σὺν ἡμῖν δοξάζωσι...

WATU Amina. — Ἀμήν.

SHEMASI Walio wakatihumeno, tokeni. Enyi wakatihumeno, tokeni. Walio wakatihumeno, tokeni. Mtu mkatihumeno asikae ndani. — Ὅσοι κατηχούμενοι, προέλθετε.

B

LITURGHIA YA WAUMINI

SHEMASI Sisi tulio waumini, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana. — Ὅσοι πιστοί. Ἔτι...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, Ee Mungu, kwa neema yako.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Hekima.

Halafu ya kufungua Antiminsio

Maombi ya kwanza ya waumini

KASISI *kwa mnong'ono*

Tunashukuru,Ee Bwana,Mungu wa majeshi,uliyetustahilisha hata sasa kusimama mbele ya madhabahu matakatifu na kusujudu mbele zako,tukiomba huruma yako kwa ajili ya dhambi zetu na ya makosa ya watu ya kutokusudia; Ee Mungu, upokee maombi yetu; utustahilishe kukuletea maombi, dua na sadaka bila damu, kwa ajili ya watu wako wote; utuwezeshe, sisi uliotuweka katika utumishi huu kwa uwezo wa Roho wako Mtakatifu, ili tukuitao wakati wote

Εὐχαριστοῦμέν σοι, Κύριε, ὁ Θεός...

na katika mahali po pote, bila hatia na bila karipio, ila katika ushuhuda na dhamiri yetu safi; ili ukitusikiliza sisi utufadhili kadiri ya wingi wa wema wako.

kwa sauti

Kwa kuwa utukufu wote, na heshima, na usujudu ni haki yako, ya Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele. ῞Οτι πρέπει σοι...

WATU Amina.

SHEMASI Tena na tena kwa amani tumwombe Bwana.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, Ee Mungu, kwa neema yako. Ἀντιλαβοῦ, σῶσον,...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Hekima. Σοφία.

Maombi ya pili ya waumini

KASISI *kwa mnong'ono*

Tena na tena tunakusujudu na kuku- Πάλιν καὶ πολλάκις σοί...

omba, wewe uliye mwema na mpenda-
wanadamu, ili ukiangalia maombi
yetu usafishe roho zetu na miili
yetu na kila unajisi wa mwili na
waroho; tena utupe kusimama mbele
ya madhabahu yako bila hatia na
hukumu. Hata uwape hao waliosali
pamoja nasi maendeleo ya maisha,
na imani, na hekima ya roho; uwa-
jalie kukuabudu daima kwa hofu na
upendo; tena kushiriki ushirika
wako takatifu bila hatia na hukumu,
hata wastahilishe kuingia katika
ufalme wako wa mbinguni juu.

kwa sauti

Ili sisi tukilindwa daima kwa ku-
tawala kwako, tutoe utukufu, kwa
Baba, na Mwana, na Roho Mtakati-
fu, sasa na sikuzote, hata mile-
le na milele.

Ὅπως ὑπό τοῦ κράτους σου...

WATU Amina.

KUINGIA KUBWA

Wimbo wa Waheruvi (Heruviko)

Οἱ τά Χερουβείμ...

WATU Kama Waheruvi, sisi kwa siri tuna-

ofanana na tunaoimbia Utatu mpaji wa uhai wimbo wa takatifu tatu (Wimbo Trisaghio), tuweke mbali kila tafakari ya maisha.
Kwa kuwa tutamkaribisha Mfalme wa wote.

Sala ya wimbo wa Waheruvi

KASISI *kwa mnong'ono*

Mtu wa tamaa na anasa za mwili hastahili kukujia au kukukaribia na kukuabudu, Ee Mfalme wa utukufu; kwa kuwa kukutumikia ni kwa hofu sana, hata kwa majeshi ya mbinguni. Lakini, kwa kuwa unawapenda wanadamu kwa hali ya ajabu, umejifanya mtu na kuwa kuhani Mkubwa wetu bila kujigeuza au kutobadilika; na wewe ndiwe umetupatia kuadhimisha dhabihu hii isiyo na damu, wewe uliye Bwana wa Mabwana wa vitu vyote. Kwa kuwa ndiwe, Bwana, Mungu wetu, pekee watawala vilivyo mbinguni na duniani, unayeketi katika kiti cha enzi begani mwa Wa- Οὐδείς ἄξιος...

heruvî, uliye Bwana wa Maṣerafî tena mfalme wa Israeli; ndiwe mtakatifu pekee, uliyepumzika kati ya watakatifu. Basi nakusihi wewe, uliye Mwema pekee na kusikia rahisi; uniangazie mimi mtumwa wako mwenye dhambi na asiyefaa; utakase roho na moyo wangu na kila dhamiri mbaya; tena unijalie kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ili, nikivaa neema ya ukasisi, nisimame mbele ya Meza yako hii takatifu, na kuadhimisha Mwili wako mtakatifu na wa usafi na Damu yako ya thamani. Kwa kuwa nakujia wewe, nikiinama shingo yangu, nikakusihi: Usinifiche uso wako, na usinikatae kuwa miongoni mwa watumwa wako; bali, mimi mtumwa wako mwenye dhambi nisiyestahili, unistahilishe kukuletea vipaji hivi. Kwa kuwa wewe ndiwe uliyetoa tena uliyetolewa, uliyepokea tena uliyegawanywa, Ee Kristo, Mungu wetu, na kwako tunatoa utukufu, pamoja na Baba yako

asiye na mwanzo, na kwa Roho Mtakatifu kamili, mwema na mpaji wa uhai, sasa na sikuzote, hata milele na milele. Amina.

Baadaye kasisi na shemasi wanasema kwa mnong'ono sawasawa mara tatu hivi

KASISI Kama Waheruvî kwa siri tunaofanana na tunaoimbia Utatu mpaji wa uhai wimbo wa takatifu tatu (Wimbo Trisaghio), tuweke mbali kila tafakari ya maisha. Οἱ τά Χερουβείμ...

SHEMASI Kwa kuwa tutamkaribisha Mfalme wa wote, akifuatwa na majeshi ya Malaika kwa kutoonekana. Alleluia, Alleluia, Alleluia. Ὡς τόν βασιλέα τῶν ὅλων...

Kasisi anafukiza akisema kwa mnong'ono

Tukiwa tumeona ufufuko wake Kristo tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye pekee bila dhambi. Tunasujudu msalaba wako, Ee Kristo, tena tunasifu na kutukuza ufufuko wako takatifu. Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu

wetu, tunajua wewe pekee, hatumjui mwengine, jina lako tunaliita. Njoni, enyi waumini wote, tusujudu ufufuko mtakatifu wa Kristo. Kwa kuwa kwa msalaba furaha umefika katika dunia yote. Tukimhimidi Bwana sikuzote, tunasifu utukufo wake; kwa sababu akivumilia msalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

Kama ni siku za wiki zisizo Jumabwana, anasema

Njoni, tumwinamie na tumsujudu Mungu mfalme wetu. Njoni, tumwinamie na tumsujudu Kristo yu Mungu mfalme wetu. Njoni, tumwinamie na tumsujudu yeye Kristo, aliye mfalme na Mungu wetu.

Baadaye anasema Zab.51..
Halafu kasisi na shemasi wakainama mbele ya Meza takatifu mara tatu wakisema katika kila mwinamo:

Ee Mungu, uniwie radhi, mimi, mtu mwenye dhambi.

Mwisho wakipinduka kwa mkutano wa-

nainama mbele ya watu wote

Baadaye

SHEMASI Ee Padri, inua. — Ἔπαρον, Δέσποτα.

KASISI Painulieni patakatifu mikono yenu, na kumhimidi Bwana. — Ἐπάρατε τάς χεῖρας ὑμῶν...

Baadaye wanafanya Kuingia Kukubwa

SHEMASI Bwana Mungu, atukumbuke sisi sote katika ufalme wake, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Πάντων ἡμῶν μνησθείη...

Kasisi vile vile.

WATU Amina.

Shemasi anapoingia anamwambia kasisi kwa mnong'ono

SHEMASI Bwana Mungu akumbuke ukasisi wako katika ufalme wake, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Τῆς ἱερωσύνης σου μνησθείη...

Na kasisi anamwambia shemasi sawasawa, kwa mnong'ono

KASISI Bwana Mungu akumbuke ushemasi wako katika ufalme wake, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Τῆς διακονίας σου...

WATU Akifuatwa na majeshi ya Malaika kwa kutoonekana.
Alleluia, Alleluia, Alleluia.

Ταῖς ἀγγελικαῖς...

KASISI *akiweka Vipaji Vitakatifu juu ya Meza takatifu anasali*

Mheshimiwa Yosefu alipotoa Mwili wako mtakatifu kutoka msalabani, aliuweka kwa shiti safi na manukato mazuri akaulaza na akauweka katika kaburi mpya.

Ὁ εὐσχήμων Ἰωσήφ...

Ee Kristo, ulikuwa kaburini na Mwili wako, lakini kuzimuni na moyo, kwa kuwa wewe ndiwe Mungu; tena ulikuwa Paradiso pamoja na mnyang'anyi, ukijaza vitu vyote, wewe ndiwe usiye na mwisho.

Ee Kristo, jinsi kaburi yako, iliyo chemchemi ya ufufuo wetu, jinsi ilionyeshwa kuwa mpaji wa uhai na mzuri kuliko Paradiso na chumba cha mfalme cha fahari kweli!

SHEMASI Ee Padri, utende mema.

KASISI *akifukiza Vipaji Vitakatifu*

Ndipo watakapotoa ng'ombe, juu ya madhabahu yako. *(3)*

Τότε ἀνοίσουσιν...

kisha anamwambia shemasi

Unikumbuke, ee ndugu yangu tunao-adhimisha pamoja nami.

Μνήσθητί μου, ἀδελφέ καί...

SHEMASI Bwana Mungu akumbuke ukasisi wako katika ufalme wake, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

Uniombee, ee Padri mtakatifu.

Τῆς ἱερωσύνης σου μνησθείη...

KASISI Roho Mtakatifu atakuja juu yako,na nguvu zake aliye juu zitakufunika kama kivuli.

Πνεῦμα ἅγιον...

SHEMASI Roho Mtakatifu huu ataadhimisha pamoja nasi siku zote za maisha yetu.

Unikumbuke, ee Padri mtakatifu.

Αὐτό τό Πνεῦμα...

KASISI Bwana Mungu akumbuke utumishi wako katika ufalme wake, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

Τῆς διακονίας σου μνησθείη...

SHEMASI Amina.

MAOMBI (SYNAPTI) YA VIPAJI VITAKATIFU

SHEMASI Tumalize maombi yetu kwa Bwana. Πληρώσωμεν τήν...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa vilivyowekwa mbele, tumwombe Bwana. Ὑπέρ τῶν προτεθέντων...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya nyumba hii takatifu, na waingiamo kwa imani, kwa heshima na kwa kumcha Mungu, tumwombe Bwana. Ὑπέρ τοῦ ἁγίου Οἴκου...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, ghadhabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana. Ὑπέρ τοῦ ῥυσθῆναι...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi kwa neema yako, Ee Mungu. Ἀντιλαβοῦ, σῶσον,...

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

SHEMASI Siku hii yote iwe kamili, takatifu Τήν ἡμέραν πᾶσαν,...

tulivu na bila dhambi, tuombe kwa Bwana.

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya kuwa na malaika wa amani, mwongozi mwaminifu, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana. ῎Αγγελον εἰρήνης,...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya msamaha na maondoleo ya dhambi zetu na makosa yetu, tuombe kwa Bwana. Συγγνώμην καί ἄφεσιν τῶν ἁμαρτιῶν...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya vitu vyema vifaavyo kwa roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana. Τά καλά καί συμφέροντα ταῖς...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya kumaliza maisha yetu yanayobaki kwa amani na toba, tuombe kwa Bwana. Τόν ὑπόλοιπον χρόνον τῆς ζωῆς...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Tuombe ili mwisho wa maisha yetu uwe kikristo kwa amani, bila maumivu, aibu, tena tuone teto njema Χριστιανά τά τέλη τῆς ζωῆς ἡμῶν,...

mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Tumkumbuke Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa zaidi kushinda wote, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu na Bikira daima, pamoja na watakatifu wote, hata sisi pia wenyewe na kila mmoja wetu na wenzetu wote, hata maisha yetu ,kujiweka mikononi mwa Kristo Mungu.

Τῆς παναγίας, ἀχράντου,...

WATU Kwako, Ee Bwana.

Σοί, Κύριε.

Sala ya Prothesi

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, uliye Mungu mwenye enzi na mtakatifu pekee, unayepokea dhabihu ya sifa na hawa waliokuita kwa moyo wao wote, upokee hata maombi yetu sisi tulio na dhambi, na uyaletea juu ya madhabahu yako matakatifu. Tena utujalie kukuletea vipaji na dhabihu za roho kwa ajili ya dhambi yetu na ya makosa ya

Κύριε, ὁ Θεός ὁ Παντοκράτωρ, ὁ μόνος...

mkutano. Tena utustahilishe kuona neema kwako, ili upendezwe na dhabihu yetu, na Roho mwema wa neema yako akae juu yetu na Vipaji hivi na watu wako wote.

kwa sauti

Kwa huruma za Mwana wako pekee, pamoja nawe unayehimidiwa, na Roho wako Mtakatifu kamili, mwema na mpaji wa uhai, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Διά τῶν οἰκτιρμῶν τοῦ Μονογενοῦς...

WATU — Amina.

KASISI — Amani kwa wote. — Εἰρήνη πᾶσι.

WATU — Na iwe kwa roho yako. — Καί τῷ πνεύματί σου.

SHEMASI — Tupendane sisi kwa sisi, ili sote kwa nia moja tuungame. — Ἀγαπήσωμεν ἀλλήλους, ἵνα...

WATU — Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, Utatu wa asili moja, na asiyetengana. — Πατέρα, Υἱόν,...

KASISI — *kwa mnong'ono*

Nitakupenda, Ee Bwana, nguvu zangu; Bwana ni imara yangu na boma langu, na mwokozi wangu. (3) — Ἀγαπήσω σε, Κύριε,...

SHEMASI Milango; milango; tusikilize kwa hekima. — Τάς θύρας, τάς...

Ikiri (Simvolo) wa imani wa Nikea

MSOMAJI Nasadiki Mungu mmoja, Baba, mwenyezi, mwumba wa mbingu, na wa nchi, hata vyote vilivyoonekana na visivyoonekana. — Πιστεύω εἰς ἕνα...

Tena Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, aliyezaliwa na Baba kabla ya wakati wo wote.

Nuru toka nuru, Mungu kweli toka Mungu kweli, aliyezaliwa, hakuumbwa, aliye asili moja na Baba, kwa yeye vyote vilifanywa.

Aliyeshuka mbinguni kwa ajili yetu wanadamu na ya wokovu wetu, akapata mwili kwa Maria bikira na Roho Mtakatifu, hata kuwa mtu.

Aliyesulubiwa kwa ajili yetu wakati wa enzi ya Pontio Pilato, akateswa, akawekwa kaburini.

Aliyefufuka katika siku ya tatu, kama Maandiko yanenavyo.

Aliyepaa mbinguni; ndipo anapokaa

kuume kwa Baba.
Atakayekuja mara ya pili kwa utukufu kuwahukumu wahai na wafu; na ufalme wake utakuwa bila mwisho.
Tena nasadiki Roho Mtakatifu, yu Bwana, yu mpaji wa uhai; anayetoka kwa Baba; anayesujudiwa na kutukuzwa pamoja na Baba na Mwana, aliyenena kwa midomo ya manabii.
Tena nasadiki Ekklisia moja, takatifu, katholikî na la Mitume.
Naungama ubatizo moja kwa maondoleo ya dhambi.
Natumaini ufufuo wa wafu, hata uzima wa ulimwengu utakaokuja.

WATU Amina.

SADAKA (ANAFORA) TAKATIFU

SHEMASI Tusimame wima vizuri; tusimame wima kwa hofu; tuangalie, kuletee sadaka (anafora) takatifu kwa amani. — Στῶμεν καλῶς· ...

WATU Huruma ya amani; dhabihu ya sifa. — Ἔλεον εἰρήνης,...

KASISI Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, — Ἡ χάρις τοῦ Κυρίου...

na upendo wa Mungu Baba, na ushirika wa Roho Mtakatifu, uwe na nyini nyote.

WATU Na iwe kwa roho yako. — Καί μετά τοῦ πνεύματός σου.

KASISI Tuweke mioyo juu. — Ἄνω σχῶμεν τάς...

WATU Tumeiweka kwa Bwana. — Ἔχομεν πρός...

KASISI Tumshukuru Bwana. — Εὐχαριστήσωμεν τῷ...

WATU Ni wajibu na haki. — Ἄξιον καί δίκαιον.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ni wajibu na haki kukuimbia, kukuhimidi, kukusifu, kukushukuru, kukusujudu katika mahali po pote pa utawala wako. Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu usiyeelezeka, usiyewazika, usiyeonekana, usiyechunguzika, usiye na mwanzo tangu milele, uliye sawasawa nyakati zote, wewe na Mwana wako pekee, na Roho wako Mtakatifu; wewe ulitufanya toka bure, na tukawa; na tuangukapo, wewe utusimamisha, na ulifanya vyo vyote, mpaka kutupaza mbinguni, ili kutupatia ufalme wako itakaokuja. — Ἄξιον καί δίκαιον σέ ὑμνεῖν, σέ...

Kwa ajili ya hivi vyote tunakushukuru wewe, na Mwana wako pekee, na Roho wako Mtakatifu; tunakushukuru kwa ajili ya vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana ulivyotutendea. Tunakushukuru hata kwa ajili ya Liturghia hii uliyokubali kuipokea kwa mikono yetu, ingawa wasimama mbele zako ma elfu ya Malaika majemadari, na ma elfu ya Malaika, Waheruvî na Waserafî, wenye Mabawa sita, Macho-mengi, wanapepea juu,

kwa sauti

Wakiimba na kulia, wakipaza sauti, na kusema wimbo wa shangwe. — Τόν ἐπινίκιον ὕμνον...

WATU — Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Sabaoth (wa Majeshi); nchi na mbingu zimejazwa na utukufu wako; Osanâ mbinguni juu; mhimidiwa ajaye kwa jina la Bwana; Osanâ mbinguni juu. — Ἅγιος, Ἅγιος, Ἅγιος, Κύριος...

KASISI — *kwa mnong'ono*

Hata sisi pamoja nao majeshi heri, tunapaza sauti, na kusema kwa wewe, — Μετά τούτων καί...

Ee Bwana wa Mabwana mpenzi wa wanadamu: Wewe ni Mtakatifu; Mtakatifu kamili, na Mwana wako pekee, na Roho wako Mtakatifu. Wewe ni Mtakatifu, Mtakatifu kamili, na utukufu wako adhimu; uliyependa ulimwengu wako jinsi hii, hata ukamtoa Mwana wako pekee, kusudi kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele; yeye, alipokuja na kumaliza chote kikusudiwacho na Mungu kwa ajili yetu, usiku ule alipotolewa, na zaidi alijitoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu, akichukua mkate mikononi yake mitakatifu na isiyo na doa, akashukuru, akaubariki, akautakasa, akaumega na akawapa wanafunzi na mitume wake watakatifu akisema:

kwa sauti

Twaeni, kuleni; huu ndio mwili wangu unaomegwa kwa ajili yenu, kwa maondoleo ya dhambi. Λάβετε, φάγετε,...

WATU Amina.

KASISI *kwa mnong'ono*

Sawasawa na kikombe baada ya kula akisema, 'Ομοίως καί τό...

kwa sauti

Nyweni nyote na hii; hii ndiyo damu yangu ya agano jipya, imwagikayo kwa ajili yenu na ya wengi, kwa maondoleo ya dhambi. Πίετε ἐξ αὐτοῦ...

WATU Amina.

KASISI *kwa mnong'ono*

Kwa hivyo tukikumbuka amri hii ya kuleta kuokoa, tena vyote vilivyofanywa kwa ajili yetu, msalaba,kaburi, ufufuko wa siku ya tatu, kupaa mbinguni, kukaa kwa kuume na kuja mara ya pili kwa utikufu, Μεμνημένοι τοίνυν...

kwa sauti

Vilivyo vyako kutoka vilivyo vyako, tunavikuletea kadiri ya vyote na kwa ajili ya vyote. Τά σά ἐκ τῶν σῶν,...

WATU Tunakuimbia, tunakuhimidi, tunakushukuru, Ee Bwana, na kukuomba wewe, Mungu wetu. Σέ ὑμνοῦμεν, σέ...

KASISI *kwa mnong'ono*
Tena tunakuletea dhabihu hii ya akili na bila damu, na tunakuomba, na kukusihi, na kukurongaronga: Utume Roho wako Mtakatifu juu sisi na juu ya Vipaji hivi ilivyo mbele.
῎Ετι προσφέρομέν σοι...

SHEMASI Ee Padri, bariki mkate mtakatifu.
Εὐλόγησον, Δέσποτα, ...

KASISI Na ufanye mkate huu kuwa Mwili mheshimiwa wa Kristo wako.
Καί ποίησον τόν μέν...

SHEMASI Amina.
Ee, Padri, bariki kikombe kitakatifu.
Εὐλόγησον, Δέσποτα, ...

KASISI Na iliyo ndani ya kikombe hiki kuwa Damu heshimiwa ya Kristo wako.
Τό δέ ἐν τῷ Ποτηρίῳ...

SHEMASI Amina.
Ee Padri, bariki Vitakatifu vyote viwili.
Εὐλόγησον, Δέσποτα, ...

KASISI Kwa kuvigeuza kwa Roho wako Mtakatifu.
Μεταβαλών τῷ Πνεύματί σου τῷ Ἁγίῳ.

SHEMASI Amina; Amina; Amina.

KASISI *kwa mnong'ono*
Ili vitakuwa kwa hao wanaovipokea
῞Ωστε γενέσθαι τοῖς...

kuwaletea makesha ya roho, maondoleo ya dhambi, ushirika wa Roho wako Mtakatifu, utimilifu wa ufalme wa mbinguni, uthabiti mbele yako, bila kuwa na hatia au hukumu. Tena tunakuletea dhabihu hii ya akili kwa ajili yao waliorehemiwa katika imani, Mababu, Mababa, Wapatriarkha, Manabii, Mitume, Wahubiri, Mashahidi, Waungama, Watawa, na kila roho ya mwenye haki aliyemalizika katika imani.

kwa sauti

Kwa ajili ya Maria Mtakatifu kamili, asiye na doa, mbarikiwa zaidi kushinda wote, Bibi wetu mtukufu, Mzazi-Mungu (Theotokos) na Bikira daima. Ἐξαιρέτως τῆς παναγίας, ἀχράντου,...

WATU Ni wajibu kweli kukuita heri, Ee Mzazi Mungu (Theotokos), mbarikiwa daima na bila doa tena Mama wa Mungu wetu. Uliye wa thamani kushinda Waheruvî, unaye utukufu kupita bila kiasi Waserafî, uliyemzaa Mungu Neno bila kuharibika, uliye Ἄξιόν ἐστιν ὡς...

Mzazi-Mungu (Theotokos) kweli, tunakukuza we.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ya Yohana nabii, mtangulizi na mbatizaji; ya mitume watukufu na wasifiwa kamili; ya *(jina la mtakatifu wa siku)* anayekumbukwa siku hiyo; hata ya Watakatifu wako wote; kwa maombi yao utujie, Ee Mungu. Na ukumbuke wote hawa waliolala katika matumaini ya ufufuo,ya uzima milele *(majina)*; na kuwarehemia mahali pa mwangaza wa nuru ya uso wako. Tena tunakusihi, ukumbuke, Ee Bwana, kila uaskofu wa waorthodhoksi, walioshika imara neno la ukweli wako, ukasisi wote, ushemasi katika Kristo, hata kila jeshi la ukasisi na la utawa. Tena tunakuletea ibada hii ya akili kwa ajili ya ulimwengu; ya Ekklisia lako takatifu, katholikî na la Mitume; ya hawa wanaoishi katika usafi na mwenendo wa kiasi; ya watawala wetu, walioamini na kumpe- Τοῦ ἁγίου Ἰωάννου,...

nda Kristo; wape kutawala katika amani, ili hata sisi tupite maisha yetu katika utulivu na shauri, kwa kila heshima ya Mungu na mwenendo mwema.

kwa sauti

Ee Bwana, ya kwanza umkumbuke Askofu wetu mkuu *(jina)* na umlinde katika Ekklisia lako takatifu, ili aishi maisha ya amani, uzima, heshima, afya na miaka kwa kushika imara neno la ukweli wako. Ἐν πρώτοις, μνήσθητι,...

SHEMASI Hata hawa walio ndani kwa fikira ya kila mmoja; tena wanaume wote na wanawake wote. Καί ὧν ἕκαστος κατά...

WATU Na wanaume wote na wanawake wote.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana, ukumbuke mji (au Monastiri) huu mahali tunapokaa, hata kila mji na nchi, na hawa wanaokaa humo kwa imani. Uwakumbuke, Ee Bwana, wasafiri hewani, baharini na nchini kavu, wagonjwa, wachoshwa na mateka, na kwa ajili ya Μνήσθητι, Κύριε, τῆς πόλεως,...

wokovu wao. Ee Bwana, uwakumbuke hawa wanaotenda matendo mema katika maekklisia yako matakatifu na wakumbukao maskini; na utuletee sisi sote huruma yako.

kwa sauti

Na utujalie sisi, ili kwa kinywa kimoja, na moyo mmoja tutukuze na kusifu jina lako adhimu na heshimiwa, la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele. Καί δός ἡμῖν, ἐν...

WATU Amina.

KASISI Rehema za Yesu Kristo, Mungu mwenye enzi na Mwokozi wetu, ziwe pamoja na ninyi nyote. Καί ἔσται τά ἐλέη...

WATU Na ziwe kwa roho yako. Καί μετά τοῦ...

UTENGENEZAJI KWA USHIRIKA

SHEMASI Baada ya kuwakumbuka watakatifu wote, tena na tena kwa amani tumwombe Bwana. Πάντων τῶν ἁγίων...

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya vipaji viheshimiwa, vilivyoletwa na kutakaswa, tumwombe Bwana. — Ὑπέρ τῶν προσκομισθέντων καί...

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Ili Mungu wetu, mpenda-wanadamu, aliyevipokea katika madhabahu yake matakatifu, yaliyo ya mbinguni juu na ya kiroho, kuwa manukato ya harufu ya kiroho, aturudishie neema ya Mungu, na karama ya Roho Mtakatifu, tumwombe Bwana. — Ὅπως ὁ φιλάνθρωπος Θεός ἡμῶν, ὁ...

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Kwa ajili ya kuokolewa na kila sikitiko, ghadhabu, hatari na uhitaji, tumwombe Bwana. — Ὑπέρ τοῦ ῥυσθῆναι...

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Utusaidie, utuokoe, utuhurumie, utuhifadhi, Ee Bwana, kwa neema yako. — Ἀντιλαβοῦ, σῶσον,...

WATU Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI Siku hii yote iwe kamili, takatifu na tulivu, bila dhambi, tuombe kwa Bwana. — Τήν ἡμέραν πᾶσαν,...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya kuwa na malaika wa a- — Ἄγγελον εἰρήνης,...

mani, mwongozi mwaminifu, mlinzi wa roho zetu na miili yetu, tuombe kwa Bwana.

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya msamaha na maondoleo ya dhambi zetu na makosa yetu, tuombe kwa Bwana. Συγγνώμην καί...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya vitu vyema vifaavyo kwa roho zetu na amani ya dunia yote, tuombe kwa Bwana. Τά καλά καί συμφέρονται ταῖς ψυχαῖς...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Kwa ajili ya kumaliza maisha yetu yanayobaki kwa amani na toba, tuombe kwa Bwana. Τόν ὑπόλοιπον χρόνον...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Tuombe ili mwisho wa maisha yetu iwe kikristo kwa amani, bila maumivu, aibu, tena tuone teto njema mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo. Χριστιανά τά τέλη...

WATU Kidhi, Ee Bwana.

SHEMASI Tukiomba umoja wa imani, na ushirika wa Roho Mtakatifu, sisi na kila mmoja mwenyewe, na wenzetu wote, Τήν ἑνότητα τῆς...

hata maisha yetu pia, tujiweke mikononi mwa Kristo Mungu.

WATU Kwako, Ee Bwana.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Bwana wa Mabwana, tunaweka maisha yetu na matumaini yetu mikononi mwako, na kukuomba, na kukusihi, na kukurongaronga; utujalie kushiriki katika fumbo (sakramenti) zako za mbinguni na za kutisha sana, za Meza hii ya ki-umungu na ya kiroho, kwa dhamira safi, tupate maondoleo ya dhambi, msamaha wa makosa, ushirika wa Roho Mtakatifu, urithi wa ufalme wa mbinguni, uthabiti mbele zako, bila kuwa na hatia au hukumu.

Σοί παρακατατιθέμεθα τήν ζωήν ἡμῶν...

kwa sauti

Na utustahilishe, Ee Bwana wa Mabwana, tukiwa na uthabiti, bila hukumu, tuwe na ujasiri kukuita Baba, wewe Mungu uliye mbinguni, na kusema:

Καί καταξίωσον ἡμᾶς, Δέσποτα,

Sala ya Bwana

MSOMAJI Baba yetu uliye mbinguni;

Πάτερ ἡμῶν,...

jina lako litukuzwe;
ufalme wako uje;
mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.
Utupe leo mkate wetu wa kila siku;
na utusamehe deni zetu, kama sisi tuwasamehevyo wadeni wetu;
tena usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.

KASISI Kwa kuwa ufalme, na nguvu, na utukufu ni wako, wa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Ὅτι σοῦ ἐστιν ἡ...

WATU Amina.

KASISI Amani kwa wote. — Εἰρήνη πᾶσι.

WATU Na iwe kwa roho wako. — Καί τῷ πνεύματί σου.

SHEMASI Tuiname vichwa vyetu kwa Bwana. — Τάς κεφαλάς ἡμῶν...

WATU Kwako, Ee Bwana. — Σοί, Κύριε.

KASISI *kwa mnong'ono*

Tunakushukuru, Mfalme usiyeonekana; kwa nguvu yako isiyopimika, umeviumba vyote, tena kwa wingi wa hu- — Εὐχαριστοῦμέν σοι, Βασιλεῦ ἀόρατε,...

ruma zako umevitoa vyote toka bure, na vikawa. Wewe ndiwe, Ee Bwana wa Mabwana, utazame toka mbinguni juu ya hawa walioinama kwako vichwa vyao; kwa kuwa hawainami kwa mwili na damu, ila kwako, uliye Mungu wa kutisha. Basi wewe, Bwana wa Mabwana, utupatie vipaji hivi vifae kila mmoja wetu kwa haja yake; usafiri pamoja nao wanaosafiri baharini, hewani na nchini; uponye wagonjwa, wewe uliye mganga wa roho na miili yetu.

kwa sauti

Kwa neema, na rehema, na upendo wa wanadamu wa Mwana wako pekee, pamoja na wewe mhimidiwa, na Roho Mtakatifu kamili, mwema na mpaji wa uhai, sasa na sikuzote, hata milele na milele. Χάριτι, καί...

WATU Amina.

KASISI *kwa mmong'ono*

Ee Bwana Yesu Kristo Mungu wetu, toka maskani yako matakatifu na Πρόσχες, Κύριε,...

toka enzini mwako mwa utukufu wa ufalme wako, uangalie, utujie na kututakasa, wewe unayekaa juu pamoja na Baba, tena hapa pamoja nasi bila kuonekana. Na ukubali kutushirikisha, kwa mkono wako, Mwili wako na Damu yako heshimiwa, na kwa mikono yetu kuwashirikisha washarika wote.

KA.-SHE. *kwa mmong'ono*

Ee Mungu, uniwie radhi, mimi mtu mwenye dhambi.

SHEMASI Tusikilize. Πρόσχωμεν.

KAŠISI Vitu Vitakatifu kwa watu watakatifu. Τά ἅγια τοῖς ἁγίοις.

WATU Mtakatifu ni mmoja pekee, Bwana ni mmoja pekee, Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu wa Mungu Baba. Amina. Εἷς Ἅγιος, εἷς...

Kila Jumabwana inaimbwa Kinoniko:

Msifuni Bwana kutoka mbinguni; msifuni katika mahali pa juu pia. Alleluia. Alleluia. Alleluia. Αἰνεῖτε τόν Κύριον...

(Kila sikukuu ina Kinonikô ya pekee).

kwa mnong'ono

SHEMASI Ee Padri, mega mkate mtakatifu. Μέλισον, Δέσποτα,...

KASISI Anamegwa na kugawanyika Mwana-kondoo wa Mungu, akatwaye kila mara bila kutengana, anayeliwa kila mara bila kumalizwa, lakini awatakasa washirika wake. Μελίζεται καί...

SHEMASI Ee Padri, jaza kikombe kitakatifu. Πλήρωσον, Δέσποτα,...

KASISI Kujawa na Roho Mtakatifu. Πλήρωμα ποτηρίου...

SHEMASI Amina.
Ee Padri, ubariki maji ya moto. Εὐλόγησον, Δέσποτα, τό

KASISI Ubarikiwe umoto wa watakatifu wako, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. Εὐλογημένη ἡ ζέσις...

SHEMASI Amin.
Moto wa Roho Mtakatifu. Amina. Ζέσις πίστεως...

Maombi ya ushirika mtakatifu

Nasadiki, Ee Bwana, na kuungama kuwa kweli ndiwe Kristo, Mwana wa Πιστεύω, Κύριε, καί...

Mungu aliyehai, uliyekuja duniani kuwaokoa wenye dhambi, kati yao ni mimi wa kwanza. Tena nasadiki kuwa huu ndio Mwili wako wa bila doa na hii ndiyo Damu yako heshimiwa. Basi nakuomba: unihurumie na kunisamehe makosa yangu, ya hiari ama yasio na hiari, kwa maneno ama kwa matendo, ninayofahamu ama nisiyofahamu; na unistahilishe kushiriki katika fumbo (sakramenti) lako la bila doa, kwa ajili ya maondoleo ya dhambi na uzima wa milele.

Tazama! Naujia ushirika wa umungu; Ἰδοὺ βαδίζω πρός...
Ee Mwumba, usinichome katika kushiriki;
Kwa kuwa u moto kuwachoma wasiostahili;
Bali unisafishe na kila doa.

Unipokee leo, Ee Mwana wa Mungu, Τοῦ Δείπνου σου...
kuwa mshiriki wa karamu yako ya fumbo (sakramenti); sitafunua kamwe fumbo lako kwa maadui wako, wala sitakubusu kama Yuda; bali kama

yule mnyang'anyi nakuungama; unikumbuke, Ee Bwana, katika ufalme wako.

Ee mtu, ogopa ukiona damu hii ya umungu; | Θεουργόν Αίμα...
Kwa kuwa ni moto, kuwachoma wasiostahili;
Mwili wa Mungu unilisha na unigeuzia umungu;
Ufanya roho umungu, na kulisha akili kwa njia ya siri.

Umenivuta, Ee Kristo nikawa na hamu yako, na umenigeuza kwa upendo wako wa umungu; bali uchome dhambi zangu kwa moto wa kiroho, na unipatie kujaa furaha yako kubwa, ili nikifurahiwa sana, niadhimishe mahudhurio yako mawili, Mwema we. | Ἔθελξας πόθῳ με,...

Faharini za watakatifu wako, jinsi nitakavyoingia, mimi nisiyestahili; kwa kuwa ningekuwa na ujasiri kuingia katika chumba cha arusi, nguo yangu isiyostahili kuwa kwa arusi | Ἐν ταῖς λαμπρότησι...

inanishtaki; hivyo malaika wange-nifunga na kunitupa nje. Ee Bwana, usafishe uchafu wa roho yangu, na kuniokoa, Ee mpenda-wanadamu.

Ee Bwana wa Mabwana, mpenda-wana-damu, Yesu Kristo Mungu wangu, na-kuomba vitakatifu hivi visiwe kwa kunihukumu kwa kuwa mimi navishi-riki bila kustahili; bali viwe kwa usafisho na utakaso wa roho hata wa mwili; tena ahadi ya uzima na ufalme ujao. Basi kwa mimi ni ve-ma kutegemea katika Mungu, kuyawe-ka kwa Bwana matumaini ya wokovu wangu.

Δέσποτα φιλάνθρωπε,...

na tena

Unipokee leo, ...

Τοῦ Δείπνου σου...

KASISI Unisamehe, ee ndugu, tunayeadhimi-sha pamoja, mimi mwenye dhambi.

SHEMASI Bwana Mungu akumbuke ukasisi wako katika ufalme wake, daima, sasa na

sikuzote, hata milele na milele.

KASISI Ee Mungu, unisamehe mimi mtu mwenye dhambi. *(3)* — Ὁ Θεός ἱλάσθητί μοι,...

Mimi *(jina)*, kasisi nisiyestahili, napewa Mwili mtakatifu na wa thamani wa Yesu Kristo, Bwana, Mungu na Mwokozi wetu, kwa maondoleo ya dhambi zangu na uzima wa milele. Amina.

Hivyo kasisi anashiriki Mkate mtakatifu.

KASISI Ee shemasi, uje. — Ἱεροδιάκονε, πρόσελθε.

SHEMASI Tazama, namjia Kristo, Mfalme asiyekufa na Mungu wetu. Ee Padri, nipe mimi *(jina)*, shemasi nisiyestahili, Mwili mtakatifu na wa thamani wa Yesu Kristo, Bwana, Mungu na Mwokozi wetu, kwa maondoleo ya dhambi zangu na uzima wa milele. — Ἰδού προσέρχομαι...

KASISI Wewe *(jina)*, shemasi mtauwa, unapewa Mwili mtakatifu na wa thamani wa Yesu Kristo, Bwana, Mungu na Mwokozi wetu, kwa maondoleo ya dha- — Μεταδίδοταί σοι (...), τῷ...

mbi zako na uzima wa milele.

Amina.

KASISI *akichukua Kikombe kitakatifu*

Tena, mimi *(jina)*,kasisi nisiyestahili, napewa Damu heshimiwa, takatifu na wa uzima ya Yesu Kristo, Bwana, Mungu na Mwokozi wetu, kwa maondoleo ya dhambi zangu na uzima wa milele.

Ἔτι μεταδίδοταί μοι (...), τῷ...

Na anakunywa mara tatu;na anabusu Kikombe kitakatifu na kusema

Hii imegusa midomo yangu na kuondoa maovu yangu na kutakasa dhambi zangu.

KASISI Ee shemasi, uje tena.

Ἱεροδιάκονε, ἔτι πρόσελθε.

SHEMASI Tena namjia. Ee Padri, nipe mimi *(jina)*, shemasi nisiyestahili, Damu heshimiwa,takatifu na wa uzima wa Yesu Kristo, Bwana,Mungu na Mwokozi wetu,kwa maondoleo ya dhambi zangu na uzima wa milele.

Ἔτι προσερχομένῳ μετάδος μοι,...

KASISI Wewe *(jina)*, shemasi mtauwa, unapewa Damu heshimiwa na takatifu ya Yesu Kristo, Bwana, Mungu na Mwokozi wetu, kwa maondoleo ya dhambi

Ἔτι μεταδίδοταί σοι (...), τῷ...

zako na uzima wa milele.

Amina.

KASISI *Baadaye*

Hii imegusa midomo yako, na kuondoa maovu yako na kutakasa dhambi zako.

Τοῦτο ἥψατο τῶν...

SHEMASI *akitayarisha Vitakatifu kwa Kikombe kitakatifu*

Tukiwa tumeona ufufuko wake Kristo tumsujudu Yesu Bwana Mtakatifu aliye pekee bila dhambi. Tunasujudu msalaba wako, Ee Kristo,tena tunasifu na kutukuza ufufuko wako takatifu. Kwa kuwa wewe ndiwe Mungu wetu, tunajua wewe pekee, hatumjui mwengine,jina lako tunaliita. Njoni, enyi waumini wote, tusujudu ufufuko mtakatifu wa Kristo.Kwa kuwa kwa msalaba furaha umefika katika dunia yote. Tukimhimidi Bwana sikuzote, tunasifu utukufo wake; kwa sababu akivumilia msalaba kwa ajili yetu, aliangamiza kifo kwa kifo chake.

Ἀνάστασιν Χριστοῦ...

Angazwa, angazwa, Ee Yerusalemu mpya; kwa kuwa utukufu kwa Bwana umekuzukia wewe; furahi sasa na kushangilia, Ee Sioni; na wewe Mzazi-Mungu (Theotokos), bila doa, changamka katika ufufuko wa Yeye uliyemzaa.

Φωτίζου, φωτίζου,...

Oh sauti yako, ya umungu, ya kupendwa na tamu! maana, Ee Kristo umetuahidi kweli kuwa nasi mpaka ukamilifu wa dahari; sauti hii tukiwa nayo kama nanga ya tumaini, twashangilia.

῏Ω θείας, ὢ φίλης,...

Oh Paskha, kubwa, takatifu, ni wewe, Kristo! Oh hekima ya Mungu, Neno na nguvu yake! utupatie kukushiriki kamili kwa siku ya ufalme wako isioisha.

῏Ω Πάσχα τό μέγα...

Ee Bwana, kwa Damu yako takatifu uzifute dhambi za watu wako waliokumbushwa hapa, kwa maombi ya Mzazi-Mungu na watakatifu wako wote.

Ἀπόπλυνον, Κύριε,...

Amina.

USHIRIKA WA WAUMINI

SHEMASI Kwa kumcha Mungu, na imani, na upendo mje. — Μετά φόβου Θεοῦ,...

Na waumini wanapewa Ushirika mtakatifu.

Kasisi (au shemasi) akimpa Ushirika mtakatifu kwa kila mmoja, anasema

Mtumwa (*au* mjakazi) wa Mungu *(jina)* anapewa Mwili na Damu ya Yesu Kristo Bwana wetu, kwa maondoleo ya dhambi na uzima wa milele. Amina. — Μεταλαμβάνει...

Wakati huu waimbaji wanaimba pole pole -mara moja au zaidi- kufuata washiriki

WATU Unipokee leo, Ee Mwana wa Mungu, kuwa mshiriki wa karamu yako ya kafumbo (sakramenti); sitafunua kamwe fumbo lako kwa maadui wako, wala sitakubusu kama Yuda; bali kama yule mnyang'anyi nakuungama; unikumbuke, Ee Bwana, katika ufalme wako[1].

---

1. Toka Jumabwana ya Paskha mpaka siku

Baada ya mwisho wa Ushirika

KASISI Ee Mungu, waokoe watu wako na kubariki urithi wako. Σῶσον, ὁ Θεός τόν...

WATU Tumeona Nuru ya ukweli; tumepata Roho wa mbinguni; tumeona imani kweli, tukisujudu Utatu asiotengwa; kwa kuwa Huyu ametuokoa. Εἴδομεν τό φῶς...

SHEMASI *kwa mnong'ono*

Ee Padri, paza. Ὕψωσον, Δέσποτα.

KASISI *kwa mnong'ono*

Ee Mungu, utukuzwe juu ya mbingu, na juu ya nchi yote uwe utukufu wako. *(3)* Ὑψώθητι ἐπί τούς...

kwa mnong'ono

SHEMASI Ee Padri, himidi. Εὐλόγησον, Δέσποτα.

KASISI *kwa mnong'ono akichukua Kikombe kitakatifu*

Mhimidiwa ni Mungu wetu, Εὐλογητός ὁ Θεός ἡμῶν.

---

kabla ya Kupaa kwake Kristo mbinguni, katika kila siku na kila Jumabwana, tunaimba wimbo huu

Shirikeni Mwili wa Kristo, onjeni chemchemi ya uzima. Σῶμα Χριστοῦ...

na kwa sauti akipindukia washarika na kuonyesha Kikombe kitakatifu

Daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Πάντοτε, νῦν καί...

WATU — Amina.

KUSHUKURU - KWENDA

SHEMASI — Simameni wima; baada ya kushiriki Fumbo (sakramenti) la umungu takatifu, bila doa, la milele, la mbinguni juu, la uzima na kuogopa kweli, tumshukuru Bwana. — Ὀρθοί· μεταλαβόντες...

Utusaidie, utuokoe, utuhurumie na utuhifadhi, Ee Mungu, kwa neema yako. — Ἀντιλαβοῦ, σῶσον,...

WATU — Bwana, hurumia (Kyirie, eleison).

SHEMASI — Tukimaliza kuomba siku hii yote iwe kamili, takatifu, tulivu na bila dhambi, sisi na kila mmoja mwenyewe na wenzetu wote, hata maisha yetu pia tujiweke mikononi mwa Kristo Mungu. — Τὴν ἡμέραν πᾶσαν,...

WATU — Kwako, Ee Bwana. — Σοί, Κύριε.

KASISI *kwa mnong'ono*

Tunakushukuru, Ee Bwana mpenda-wanadamu, mfadhili wa roho zetu kwa kuwa umetujalia tena kwa wakati huu kupokea Fumbo (sakramenti) lako la mbinguni na la uzima. Umarishe njia yetu sawasawa kwa ukweli; utegemeze sisi sote katika hofu yako; ulinde maisha yetu, uzisalimishe hatua zetu; Kwa sala na maombi ya Maria Mzazi-Mungu na Bikira daima na watakatifu wako wote.

Εὐχαριστοῦμεν σοι, Δέσποτα...

kwa sauti

Kwa kuwa wewe ni utakaso wetu na kwako tunatoa utukufu, kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

Ὅτι σὺ εἶ ὁ ἁγιασμὸς ἡμῶν, καί...

WATU Amina.

KASISI Tuende kwa amani.

Ἐν εἰρήνῃ προέλθωμεν.

SHEMASI Tumwombe Bwana.

Τοῦ Κυρίου δεηθῶμεν.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

KASISI Ee Bwana, unayebariki wanaokuhimi-

Ὁ εὐλογῶν τούς...

di na unayetakasa wanaokutegemea, waokoe watu wako na kubariki urithi wako; ulinde ujazo wa Ekklisia lako; uwatakase wanaopenda uzuri wa nyumba yako. Wewe uwape marudio ya utukufu kwa uweza wako wa umungu; tena usituache sisi tunaokutumaini. Upatie dunia yako amani, tena maekklisia yako,wakasisi, viongozi wetu, majeshi na watu wako wote; kwa kuwa kila ukarimu wema na kila kipaji kilichokamili kina toka kwako juu, uliye Baba wa nuru; na kwako tunatoa utukufu na ushukuru na usujudu, kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, sasa na sikuzote, hata milele na milele.

WATU Amina.

Jina la Bwana lihimidiwe tangu sasa hata milele. *(3)* Εἴη τό ὄνομα...

KASISI *kwa mnong'ono, mbele ya Prothesi*

Ee Kristo Mungu wetu, uliye ukamilifu wa Sheria na wa Manabii, uliye kamilisha makusudi yote ya Baba, ujaze mioyo yetu kwa furaha na Τό πλήρωμα τοῦ....

shangwe, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. Amina.

SHEMASI Tumwombe Bwana. — Τοῦ Κυρίου δεηθῶμεν.

WATU Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).

KASISI Baraka ya Bwana na huruma yake imfikie nyini, kwa neema yake ya umungu na upendo yake wa wanadamu, daima, sasa na sikuzote, hata milele na milele. — Εὐλογία Κυρίου...

WATU Amina.

KASISI Utukufu kwako, Ee Kristo Mungu, matumaini yetu, utukufu kwako. — Δόξα σοι, Χριστέ...

WATU Utukufu kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu. Sasa na sikuzote, hata milele na milele. Amina. Bwana,hurumia (Kyirie,eleison).*(3)* Ee Padri mtakatifu, bariki. — Δόξα... Καί νῦν...

KASISI *Anafanya Kumaliza (Apolisi). Kama ni Jumabwana anasema*

Aliyefufuka katika wafu — Ὁ ἀναστάς ἐκ...

na halafu

Kristo Mungu wetu wa kweli, kwa maombi ya Mzazi-Mungu mtukufu ka-

mili, Maria mtakatifu; kwa nguvu ya Msalaba wa heshima na mhuishaji; kwa ulinzi wa malaika wa mbinguni; kwa maombezi ya Yohana, Nabii, mtangulizi na mbatizaji, mheshimiwa na wa sifa; ya Mitume watakatifu, watukufu na wasifiwa; ya Mashahidi watakatifu, waheshimiwa na washindaji wazuri; ya watawa watakatifu na wenye-mungu; ya Yoakimu na Anna, mababa-mungu, watakatifu na wenye-haki; ya *(mtakatifu wa kanisa)*; ya Yohana Krisostomo takatifu, askofu mkuu na Patriarka wa Kostantinopoli; ya *(mtakatifu wa siku, ona Kalenda)* tunayemkumbuka leo, na ya watakatifu wote; atuhurumie na kutuokoa, yu Mungu mwema, mrahimu na mpendawanadamu.

Kwa maombi ya mababa wetu watakatifu, Ee Bwana Yesu Kristo Mungu wetu, utuhurumie na utuokoe. Δι' εὐχῶν τῶν ἁγίων...

WATU Amina.

KASISI Utatu Mtakatifu awalinde ninyi ᾿Αμήν.

nyote.

WATU Anayetubariki na kututakasa, Ee Bwana, umlinde kwa miaka miingi. Tόν εὐλογοῦντα...

Kasisi anawagawia watu Antidhoro akisema kwa kila

KASISI Baraka ya Mungu na huruma yake ikufikie.